# *Mambo Ambayo Hayakuwa Hivyo Tangu Mwanzo*

. . . ya siku Zake, wakifundisha mambo ambayo hayakuwa hivyo. Nadhani kama Yeye angalikuja leo, angekuta jambo lile lile: mambo ambayo hayakuwa hivyo tangu mwanzo. Kama sikuzote unataka kujua kweli ni nini, rudi kwenye mwanzo. Rudi kwenye Mwanzo, nawe unaweza kuchukua kila dini potovu na kila kweli kutoka leo hii. Ninii tu . . . Mimea yote ilianza katika Mwanzo, kwa sababu Mwanzo ndio mlango wa mbegu wa Biblia. Basi iwapo tunataka kujua ukweli ni nini, turudi kuanzia mwanzo.

2 Kama tu vile nilivyokuwa nikijaribu kusema jana usiku, Mungu anapotoa tamshi mara ya kwanza, Yeye kamwe hawezi kugeuka aache tamshi hilo. Hana budi kulidumisha kote kote. Kile alichosema katika Mwanzo ni kitu kile kile katika Ufunuo, na kote kote. Yeye ni Mungu, na hakuna lingine. Mnaona? Nayo Maneno Yake yote ni kweli.

3 Sasa, tunaona ya kwamba wakati Yesu alipokuja, Yeye aliwapata walimu ambao walikuwa wamelichukua Neno la Mungu na walikuwa wamelipotosha, kujinufaisha wenyewe. Walikuwa wamezichukua amri za Mungu na kuzipotosha zikawa kanuni ya imani.

4 Sasa, kumbukeni, kuna Muumba mmoja tu, na wote . . . Shetani si muumba. *Dhambi* ni nini? *Dhambi* ni "uovu," nao *uovu* ni "haki iliyopotoshwa."

5 Labda nitalifanya dhahiri zaidi. Wao ni . . . Ninyi ni kusanyiko lililochanganyikana. Ninyi humsikiliza daktari wenu; mimi ni ndugu yenu. Mtu kuishi na mke wake ni haki. Yeye amemwoa. Tendo lile lile na mwanamke mwingine ni mauti. Moja linaleta uhai, hilo lingine ni mauti. Mnaona? *Uovu* ni "haki iliyopotoshwa." *Uongo* ni nini? Ni "kweli iliyoelezwa vibaya."

6 Kwa hiyo hayo ndiyo Yesu alikuta. Na yale sisi sote tutakayoingilia, mradi tu tunachukua na kuongeza, ama kuondoa kutoka kwa Neno la Mungu, ni kulipotosha Neno la Mungu.

7 Kwa hiyo wakati Yesu alipokuja, Yeye alikuta kwamba wao walikuwa wamelichukua Neno la Mungu na kulipotosha, na kufanya mapokeo ya mwanadamu. Naye akasema, "Kwa nini ninyi kwa mapo- . . . mnalibadilisha Neno la Mungu?" Kwa kuchukua mapokeo yao, na kulibadilisha Neno la Mungu, wakilifanya liseme jambo ambalo kweli halikusema.

8 Tunaona ya kwamba alikuta hayo katika siku Zake, Naye angeyakuta hapa leo hii. Naye, katika Uwepo, ama, katika Utu wa Roho Mtakatifu, Mungu yeye yule ambaye amekuwapo sikuzote, akiishi katika watu Wake katika mfano wa Roho Mtakatifu, inashuhudia kupitia kwa mwaminio wa kweli, ya kwamba mwanadamu hulipotosha Neno la Mungu litoshee kanuni zao za imani, badala ya kufanya kanuni zao za imani zitoshee Neno la Mungu.

9 Ninataka mtu fulani apate Imani ya Mitume katika Biblia, kama vile tungeikariri siku hizi, "Ninaamini katika kanisa Takatifu la Katoliki ya Kirumi, ushirika wa watakatifu." Chochote kinachoshirikiana na wafu ni mizimu. "Kuna Mpatanishi mmoja tu kati ya Mungu na wanadamu, Mwanadamu Kristo Yesu." Hivyo tu. Hakuna mpatanishi mwingine. Kwa hiyo chochote . . . Wao wanayapotosha mambo, wakibuni kanuni ya Imani ya Mitume.

10 Kama mitume walikuwa na kanuni yoyote ya imani, ilikuwa ni Matendo 2:38. Yeye—yeye alikuwa . . . hicho ndicho walichohubiri sikuzote na—na kushindilia ndani ya watu. Hawana budi kumtubia Mungu na kadhalika. Hiyo ni kusema, kukiweko na kanuni yoyote ya imani katika Biblia, hiyo ingekuwa ndiyo, ambayo mitume walitumia.

11 Kwa hiyo wao . . . miongozo yao yote ya Roho Mtakatifu ilidumu pamoja na Neno. Na kama mwanadamu yeyote, ama malaika, kamwe akisema lolote kinyume na Neno, Wagalatia 1:8 ilisema, "Na alaaniwe." Haina budi kuwa ni Neno la Mungu.

12 Paulo alisema, "Kama malaika kutoka Mbinguni akija kwenu na Injili yoyote nyingine mbali na ile mliyoisikia tayari, na alaaniwe." Kwa hiyo tunaamini ya kwamba mbingu na nchi zitapita, bali Neno la Mungu halitapita, kwa sababu Neno ni Mungu. Mungu hawezi kupita. Maumbile yatapita, bali Mungu hawezi kupita.

13 Sio mahali pa mizaha, mimbara sio mahali pa mizaha. Nafikiri Neno la Mungu linapaswa kuhubiriwa kutoka hapa kwa uchaji wa—wa moyo, nasi inatupasa kukumbuka hilo. Lakini kusema hilo tu, kutoa hoja hii, maskini yule mtu mweusi, hapa mahali fulani Kusini, wakati mmoja alitoa tamshi, kasema, "Afadhali awe amesimama juu ya Neno la Mungu kuliko kusimama Mbinguni." Wakamwuliza ni kwa nini. Akasema, "Maana Mbingu na nchi pia zitapita, bali Neno la Mungu halitapita." Hiyo ni kweli. Hatuna budi kukaa kwenye Neno.

14 Yesu, hapo alipokuja, Yeye alisema, "Musa kwa sababu ya ugumu wa moyo wako alikuruhusu kumtaliki mke wako: bali tangu mwanzo haikuwa hivyo." Sasa, tunaona ya kwamba walikuwa wamezichukua amri za Mungu na kuzitangua.

15 Wakati Yesu alipokuja, Yeye aliwakuta watu wakiliangalia kanisa kwa ajili ya wokovu. Walipata kitu gani? Kanuni za

imani; kila dhehebu hujifanyia kanuni zake lenyewe. Na basi hivyo ndivyo Yeye aliwakuta watu wakilitegemea kanisa kwa ajili ya wokovu; nao wakapata kanuni za imani za kujibunia.

16 Basi akija leo Yeye Mwenyewe na kuzungumza nasi, atapata kitu kile kile: mwanadamu akilifanya Neno la Mungu litoshee dhehebu lao, akiwapa kanuni za imani. Wala hakuna wokovu katika kanuni za imani, kama si Biblia. Haina budi kuwa ni Biblia, kwa sababu Neno Lake ni . . . yote tunayohitaji, ni Neno Lake. Nalo Neno Lake, wakati Yeye akiwa ni Neno, Neno la Mungu ni Mungu. Hivyo tu. Ni Neno Lake, Mwenyewe. Yeye ni . . . "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Nalo Neno lingali ni Mungu. Lingali ni Mungu.

17 Sasa, tunaona ya kwamba Yeye alipokuja, aliwakuta watu, basi, wakizichukua amri za Mungu na kuzitangua, kwa kuzichukua amri za Mungu, na kuzipatanisha na kanuni zao za imani, kwa hiyo zilitanguka. Nalo kanisa likaangalia . . . Watu walitegemea kanisa badala ya kulitegemea Neno la Mungu. Kwa hiyo basi, Yeye alisema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo."

18 Tunaliona vile vile siku hizi, kama vile nimenukuu mara mbili ama tatu tayari asubuhi ya leo, na kuangalia ile saa ya ukutani, inanitia wasiwasi, kwa hiyo ni—ninataka kusema hivi hata hivyo, ya kwamba, "Hii ni kweli." Basi katika siku hizo kama ilivyo sasa, na sasa kama ilivyokuwa wakati huo, wao wanapiga mayowe, "Mungu yuko wapi?"

19 Vema, jambo lenyewe, ni kwamba, wamemwacha Mungu hapo walipoliacha Neno Lake. Hiyo ndiyo sababu mambo yako jinsi yalivyo siku hizi, ni kwa sababu watu waliliacha Neno la Mungu.

20 Kama daktari aliandika maelekezo, maagizo ya matumizi ya dawa, nawe ukaongezea kitu kwake, ama ukaondoa mengine kwake, ungemwua mgonjwa wako. Hiyo ni kweli. Inakupasa kuyahifadhi jinsi tu yalivyoandikwa. Kuna kiuasumu cha kutosha mle kuivuruga hiyo sumu, sumu ya kutosha kuua kijidudu. Na sumu nyingi kupita kiasi ndani yake pasipo na kiuasumu ingemwua mgonjwa; na—na kiuasumu kingi kupita kiasi pasipo na sumu, kingefanya nini? Kisingemsaidia mgonjwa wako. Kwa hiyo huna budi kuyaweka sawa.

21 Na hivyo ndivyo Neno la Mungu lilivyo. Ni Maelekezo ya dawa ya Mungu. Naam, ndugu. Ni Maelekezo ya dawa ya Mungu kwa watu Wake kuponya kila maradhi, kila ugonjwa. Dhambi na mambo ya mwili, chochote kile, yote yanatatuliwa katika Neno la Mungu. Amina. Ni Neno la Mungu. Ilikuwa hivyo hapo mwanzo; Ilikuwa hivyo katika zile enzi za kati; ndivyo ilivyo katika kila wakati; na ndivyo ilivyo asubuhi hii, jinsi tu ilivyokuwa hapo Yeye alipolinena, maana haliwezi kuhitilafiana kwa chembe moja, kwa sababu ni Neno la Mungu.

22 Basi watu siku hizi, si ajabu wanapayuka: "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu." Kwa nini wanafanya hivyo? Kwa sababu wamelichukua Neno la Mungu na kulifunganisha na kanuni zao za imani, nao wamekichanganya kitu hicho vibaya. Wala hawana nguvu zozote mle. Kama malaika, askofu, askofu mkuu, ama chochote kile, akija na kubadilisha Neno moja, hiyo itabadilisha Maelekezo yote ya dawa. Hebu tukae jinsi lilivyosema hasa. Kile Mungu alichosema, hebu na tukiache moja kwa moja namna hiyo.

23 Makanisa yamekwisha siku hizi. Yako kwenye hamaki fulani mahali fulani, yakifanya mashirika, yakiunda madhehebu, yakiwafanya watu kufuata kanuni za imani badala ya kumfuata Kristo. Sitaki kanuni yoyote ya imani bali Kristo, sheria yoyote bali upendo, wala kitabu chochote bali Biblia. Hayo ndiyo tuliyo nayo hasa: Hiyo ndiyo Kanuni ya Imani ya Mungu, ndiyo Maelekezo ya dawa ya Mungu. Ni Kiuasumu cha Mungu kwa ajili ya dhambi. Ndiyo Kiuasumu cha Mungu kwa ajili ya uponyaji wetu, na Ndiyo—Ndiyo nguvu za Mungu zilizodhihirishwa kwetu, tunapolichukua Neno maishani mwetu.

24 Sasa, tunaona ya kwamba wanajibu, wanapayuka, "Yuko wapi Mungu wa Musa?" Sababu ya Musa kukaa pamoja na Mungu na kadhalika ilikuwa, Mungu alikuwa akiyafuata maelekezo ya Musa, Musa alikuwa akilifuata Neno la Mungu. Jinsi ambavyo Petro, Yakobo, na Yohana walivyolenga shabaha kila wakati, ni kwa sababu kwamba wa—walilifuata Neno.

25 Hapa wakati fulani uliopita. . .Kila mtu anajua ninapenda kulenga shabaha, na kupiga risasi, na kadhalika. Nami nilikuwa na maskini Winchester ndogo Muundo 70. Nikasimama huko nje, kwenye yadi hamsini, kwenye kituo cha kulenga shabaha, nikapiga risasi nane kwenye shimo lile lile, kwenye yadi hamsini. Ndipo ikaenda kombo kidogo, risasi. Inakubidi kujipumbaza na kuchezacheza nayo. Nami napenda kufanya hivyo, kidogo kuituliza mishipa yangu. Basi hiyo ikaenda kombo. Nisingeweza kuinyosha. Nilifikiri ilihitaji kukarabatiwa.

26 Nikairudisha kwa Kampuni ya Winchester. Wakajibu, na kusema, "Loo, Ndugu Branham, ama, Bw. Branham," wakasema, "kama. . .hiyo Winchester ni moja ya zilizo bora sana." Kasema, "Itapoteza inchi moja kwenye yadi hamsini, kwenye yadi ishirini na tano, namaanisha, inchi moja kwenye yadi ishirini na tano." Kasema, "Hiyo ndiyo nzuri sana utakayoweza kupata kwake."

27 Nilijua tofauti. Nilijua kwenye yadi hamsini nilipiga shabaha nane za moja kwa moja nayo. Kwa hiyo nilijua hiyo haikuwa kweli. Sasa, hivyo ndivyo. . .Nami nisingetulia mpaka niliporudishiwa. Sasa, itafanya jambo lile lile.

28 Sasa, mimi si mmoja wa watu hawa wanaopenda kuwa kigeugeu, "Kanisa linasema hivyo, kwa hiyo hebu na tudumu nalo." Kama wale mitume, kwa Neno la Mungu, kwa amri za Mungu, kwa Roho Mtakatifu yule yule tuliye naye, walilenga shabaha kwenye uponyaji wa Kiungu, kwa nguvu za Mungu, kama tutadumu nalo, tunajua ndivyo ilivyo hapo, kwa hiyo tutakaa hata tutakapoulenga kikamilifu, hivyo tu, kwa kuwa tunajua ilitendeka wakati mmoja.

29 Vipi kuhusu, "siku za miujiza zimepita," na "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele"? Mungu huyo anawezaje kuwa mfu ambaye alifufuka tena, na yu hai milele? Tunawezaje kulifanya kanuni ya imani, wakati Mungu hana kanuni ya imani?

30 Mungu ni Mtu. Mungu anaishi ndani ya Kanisa Lake, nanyi ndio Kanisa Lake. Kama umezaliwa mara ya pili, na kujazwa na Roho Mtakatifu, wewe ni Kanisa la Mungu. Mungu anaishi ndani ya ninii yako. . .Anafanya maskani pamoja na wewe. Mungu aliposhuka chini, akafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, Yeye alifanya nini? A—alitandaza hema Lake miongoni mwa wanadamu. Yeye—Yeye alibadilisha sifa Yake kutoka Mungu akawa mwanadamu, ili mwanadamu aweze kuwa kama Yeye. Loo, Yeye alifanyika mimi, ili kwamba kupitia kwa neema Yake niweze kufanyika Yeye.

31 Loo, ni jambo kuu jinsi gani. Kamwe hatutafahamu kwamba ilikuwa ni kitu gani. Si ajabu watu wanapayuka siku hizi, "Yuko wapi Mungu?" Rudini kwenye Neno. Rudini kwenye mwanzo.

32 Hapo mwanzo Yeye aliwaambia wanafunzi Wake, "Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hilo lilitosha. Rudini kwenye Neno lilo hilo nalo litazaa kitu kile kile. Wao walilifuata Neno hilo, Nalo likalenga kikamilifu na kupiga shabaha. Kila shabaha, kila ahadi ambayo Mungu alifanya, ilidhihirishwa.

33 Kama tutarejea kwenye Neno lilo hilo, litalenga shabaha zile zile, lifanye miujiza ile ile, lifanye mambo yale yale, lifanye maisha yale yale, lifanye kiumbe kile kile, lifufue wafu, liwaponye wagonjwa, liwatoe pepo, lione maono, litabiri. Ni Injili ile ile iliyolenga shabaha wakati huo, endapo tutarejea kwenye iyo hiyo.

34 Kama vile, kuirudisha bunduki katika hali ile ile iliyokuwa hapo mwanzo, mitetemeko yote ikikwisha, italenga risasi hiyo moja kwa moja. Basi tukiiondoa mitetemeko yote ya kutokuamini ndani yetu, Neno la Mungu litalenga kikamilifu vile vile hasa lilivyofanya hapo mwanzo. Hiyo ni kweli kabisa. Litalenga kikamilifu kila wakati. Lilifanya hivyo wakati mmoja; litafanya tena. Usiridhike na kanuni ya imani ama kitu fulani. Dumu papo hapo mpaka Neno litakapolenga shabaha kikamilifu.

35 Inanikumbusha wakati ambapo mama na baba, ama, baba wa kambo wa Bwana wetu Yesu walipokuwa wamempeleka kwenye sikukuu ya Pentekoste. Ndipo wakafanya safari ya siku tatu, na—na hatimaye wakamkosa. Wa—wasingeweza kumpata.

36 Hivyo ndivyo kanisa limeenda sasa. Limeenda zaidi . . . limefanya safari ya yapata miaka elfu mbili, nao wakamkosa. Hili hapa. Kuna ishara kila mahali zinazotokea za Kuja Kwake, nao wanasema, "Yuko wapi Mungu? Yuko wapi Mungu? Ilikuwaje Kwake?"

37 Hivi mliona? Mariamu na Yusufu walimtafuta miongoni mwa jamaa zao, bali hawakumpata. Leo hii tunarudi nyuma kuona kama Wamethodisti wanaye, Wabaptisti wanaye, Wapresbiteri, ama Walutheri. La, bwana, hawakumpata. Wala sisi hatutampata leo hii. Haijalishi ni jinsi gani tunavyojaribu kurudi nyuma na kulifufua moja la hayo madhehebu ya kale, yaliyokufa, kamwe hatutafanikiwa.

38 Walimpata wapi? Mahali walipomwacha. Haleluya! Mnafikiri mimi ni mtakatifu anayejibingirisha; nadhani ndivyo nilivyo. Mtampata tu kama wao walivyompata: mahali walipomwacha. Mahali walipomwacha, hapo ndipo walipompata. Hapo ndipo kanisa litakapompata.

39 Walimwacha wapi? Kwenye sikukuu ya Pentekoste. Kanisa litampata wapi? Kule nyuma katika sikukuu ya Pentekoste, ambako walimwacha wakati walipojiondoa kwenye fundisho la mitume na kadhalika. Huko nyuma katika nyakati hizo za mwanzoni huko nyuma, waliondoka kwake na kufanya kanuni zao wenyewe za imani, na kuanzisha fundisho la Nikolai, wakaunda kanisa Katoliki, wakaunda dhehebu la—la inayoitwa dini ya Kikristo. Na kutoka hapo wameunda madhehebu, na kuvunjilia mbali vitu hivyo, na kuwaleta Wakristo wote katika kanuni za imani, na kadhalika, na kuchanganya yote mpaka ni bonge tu lile lile ambalo Yeye alipata hapo alipokuja. Ni kweli kabisa.

40 Turejee hapo mwanzo mahali tulipomwacha, ambapo Yeye alikuwa na nguvu, wakati alipowafufua wafu, na kuwaponya wagonjwa, na kuwatoa pepo; hiyo ni kurudi moja kwa moja hadi mwanzo, mahali tulipomwacha Yeye.

41 Wao wanasema, "Yeye yuko wapi? Yeye yuko pamoja na Wamethodisti? Yeye yuko pamoja na Wabaptisti?" Ama hata, "Yeye yuko pamoja na Pentekoste?" La, bwana. Rudini kwenye asil- . . . sio shirika la Kipentekoste, dhehebu la Kipentekoste, hilo ni jina. Ni nani anayeweza kuiundia Pentekoste dhehebu? Niambieni. Pentekoste si dhehebu. Pentekoste ni tukio kwa mwaminio yeyote anayetaka kuipokea. Rudini kwenye tukio, sio kurudi kwenye dhehebu, bali kurudi kwenye tukio. Pentekoste ni tukio.

42 Hebu niwaambieni jambo fulani. Hebu angalieni lile tunda ambalo makanisa ya Kipentekoste yanazaa siku hizi, mtaona hayakuanzia hapo mwanzo: kubishana, kuzozana, hamaki, juu chini, wakishindania *hili*, na kushindania *lile*. Yesu alisema katika Yohana 14, ama Yohana 15, "Mimi Ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Hiyo ni kweli?

43 Sasa, ninyi wakulima, ninyi Wateksasi, Walouisiana, na wowote wale mliopo hapa, mtu yeyote aliye na akili timamu, aliyepata kuona mzabibu ukikua, alijua ya kwamba mzabibu hauzai tunda. Matawi ya mzabibu ndiyo yanayozaa tunda, bali linapata uhai wake kutoka kwa mzabibu. Yesu ndiye chanzo chetu cha Uzima. Naam, bwana. Sasa, tutaona, basi, kama Yesu ndiye chanzo cha Uzima wetu, basi Yeye ndiye Mzabibu wa kweli. Uhai wenyewe ulio katika mzabibu uko kwenye tawi. Basi kama mzabibu huo ukizaa tawi la kwanza, na kwenye tawi hilo mna kichala cha zabibu zinazotokeza kwake. Kama ukipata kuzaa tawi lingine, litakuwa ni kichala cha zabibu. Likizaa tawi lingine, litakuwa ni kichala cha zabibu. Nalo litakuwa tawi la aina ile ile hata mwishoni mwa huo mzabibu. Ee Mungu.

Sasa, ninahitaji nusu saa yangu; ndio ninajiandaa tu kulifikia. Amina.

44 Kila wakati mzabibu huo unapozaa tawi lingine, litakuwa kama lile tawi la kwanza. Kwa nini? Kwa sababu uhai uliomo ndani ya huo mzabibu utazaa tawi la aina ile ile. Kama mzabibu wa kwanza ulizaa zabibu, huo mwingine hautazaa maboga. Linalofuata halitazaa tunda la aina ya mchungwa. Halafu basi, baada ya kitambo kidogo, moja kwa moja namna hiyo, halitafanya hivyo.

45 Kama Mzabibu wa kweli ukizaa tawi, na kama . . . Yesu ndiye Tawi katika wa kwanza, ama, Mzabibu. Nalo tawi la kwanza lililozaa, wao waliandika Kitabu cha Matendo nyuma yake. Hiyo ni kweli? Kanisa la Kipentekoste, kanisa halisi la Kipentekoste, basi likaandika Kitabu cha Mitume, pamoja na ishara na maajabu yakimfuata mwaminio. Kama Mzabibu ule halisi wa kweli ukizaa tawi lingine, wao wataandika kitabu cha Matendo nyuma yake. Naam, bwana.

46 Hapa Arizona sio muda mrefu uliopita, nilikuwa nikiangalia mti kwenye kitalu cha mtu fulani: mti wa aina ya mchungwa. Ulikuwa na aina tisa mbalimbali za tunda kwenye mti mmoja. Ulikuwa nazo. Kila moja ya hayo lilikuwa ni tunda tofauti. Ulikuwa ni mchungwa kwanza, lakini ulikuwa na komamanga; ulikuwa—ulikuwa na malimau; ulikuwa na mabalungi; namna zote mbalimbali za tunda aina ya mchungwa. Kwa nini? Yalikuwa yamepandikizwa mle. Yalikuwa yakiishia maisha ya mti huo, bali yasingeweza kuleta chochote ila kile yalichokuwa. Yasingeweza kuleta machungwa, kwa sababu ni matawi yaliyopandikizwa. Lakini kila wakati mti huo ulipozaa tawi

jipya kutoka kwake wenyewe, ulikuwa ni mchungwa, nao ukazaa machungwa.

47 Hiyo ndiyo njia siku hizi. Tumepandikiza matawi ya Methodisti, Baptisti, Presbiteri katika Mzabibu wa kweli, nayo yanaishi kwa nguvu Zake. Bali haliwezi kuzaa kitu ila kanuni za imani na dhehebu. Lakini kama Mzabibu huo ukipata kuzaa tawi lingine, litakuwa lisiloegemea madhehebu, linalotiwa nguvu kwa Roho Mtakatifu, kama tu ilivyokuwa kwenye Siku ya—ya Pentekoste; kurejea hapo mwanzo. Amina.

Afadhali niondoke. Amina.

48 Kama Mzabibu huo ukizaa tawi lingine, litakuwa kama tu ilivyokuwa hapo mwanzo. Tunapandikiza kila namna ya kanuni za imani za kanisa ndani yake: Baptisti, Methodisti, Pentekoste, Presbiteri, Lutheri, Baptisti; na kila moja linazaa tunda la Kibaptisti, tunda la Kimethodisti, tunda la Kipentekoste, na kila kitu kingine. Lakini wakati linaporudi, kama Mzabibu huo kamwe ukizaa tawi lingine, litazaa tunda la Roho Mtakatifu. Amina. Litaninii . . .

Wao wanasema, "Vema, sisi ni Wamethodisti."

"Tangu mwanzo haikuwa hivyo."

"Sisi ni Wabaptisti."

"Tangu mwanzo haikuwa hivyo."

"Sisi ni Presbiteri."

"Tangu mwanzo haikuwa hivyo."

"Hatuamini katika kunena kwa lugha."

"Tangu mwanzo haikuwa hivyo."

"Hatuamini katika uponyaji wa Kiungu kanisani mwetu."

"Tangu mwanzo haikuwa hivyo." Haleluya! Tunachohitaji leo hii ni kitu fulani kitakachorudi hapo mwanzo tena, kurejea hapo mwanzo. Haleluya!

Wakati wangu umekwisha. Na tuombe.

49 Bwana Yesu, loo, jalia niishi kuiona ile siku ambapo kanisa litarejea hapo mwanzo. Lijalie, Bwana. Jaza mahali hapa padogo asubuhi ya leo. Mpake mafuta maskini mchungaji huyu hapa, Bwana, na hawa wengine. Tupe utukufu Wako. Tupe neema Yako. Tupe mkutano hapa, Bwana.

50 Jalia tusahau kuhusu mambo mengine na turudi hapo mwanzo, kwa kuwa tunajua kwamba Bwana wetu anazungumza ndani ya mioyo yetu asubuhi ya leo. Ondoa matawi haya yaliyopandikizwa kutoka pale. Jitenge na kutokuamini. Rudi kwenye mwanzo. Hapo ndipo ilipokuwa hivyo. Pia, Bwana, tunataka kila kitu kiwe hivyo tangu mwanzo.

51 Bwana, jalia ujuzi wetu, kama tumewahi kuwa nao hata kufikia asubuhi ya leo . . . Kukiweko na mtu fulani anayeketi

hapa ambaye kamwe hajapata kuwa na ujuzi wa Roho hiyo ya mwanzoni, na kunaye Roho yuyo huyo aliyemwagwa hapo mwanzo, kwa nini tuchukue kibadala? Kwa nini tuchukue kitu cha kilokole? Kwa nini tuchukue kanuni ya imani ya kimapinduzi, baridi, ya kawaida, isiyojali, wakati mbingu za Kipentekoste zimejaa kitu kilicho halisi sana? Kwa nini kuchukua kibadala?

52 Bwana, jalia turudi nyuma hapo mwanzo, na kumpokea kama walivyofanya hapo mwanzo, na kufanya kazi zile zile, ishara, maajabu ambayo huzaa tunda lile lile: upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, upole, unyenyekevu, saburi. Lijalie Mungu. Utusikie, Baba, kwa kuwa tunalikabidhi maskini kanisa hili na uamsho huu Kwako mkononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu awabariki. Ninachukia kulazimika kuharakisha, bali ni baada ya saa tano sasa. Nitawaona usiku wa leo. Asante . . .

61-0119M Mambo Ambayo Hayakuwa Hivyo Tangu Mwanzo
American Legion Hall
Beaumont, Texas Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org